

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA MARA

Anwani ya Simu: "REGCOM" MUSOMA
Simu Nambari +255 28
2622305/2622004/2622005
Faksi: +255 28 2622764/2622324
E-mail: ras.mara@pmoralq.go.tz



**OFISI YA MKUU WA MKOA
S.L.P. 299
MUSOMA
TANZANIA.**

Namba ya Kotesheni: *RAS/010/2017/2018/HQ/N/06*

Kwa ajili ya: **ZABUNI ZA UTOAJI HUDUMA ZA USAFI NA ULINZI
KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

MWALIKO WA KOTESHENI

Kwa:

.....

.....

.....

Tarehe: **09 Juni, 2017**

1. Mwaliko huu wa Kotesheni unafuata Tangazo la jumla la Ununuzi kwa ajili ya **Katibu Tawala Mkoa wa Mara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 unaoanzia mwezi Julai Mosi, 2017 na kuishia Juni 30, 2018.**
2. **Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara** amepokea fedha kutoka Hazina kwa ajili ya gharama za kulipia huduma ya **Ulinzi** na **Usafi** na anakusudia kutumia fedha hizo kugharamia malipo halali chini ya mikataba ambayo itatolewa katika mwaliko huu wa Kotesheni.
3. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye maelezo ya mahitaji na bei na kufafanuliwa katika sehemu II.
4. Kotesheni zote ziwe na nakala halisi na mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa Kotesheni *Na. RAS/010/2017/2018/HQ/N/06* kwa kuandika moja ya huduma anayoiomba Mzabuni kati ya hizi mbili:-
(a)Huduma ya Ulinzi
(b)Huduma ya Usafi

5. **Maelezo maalum wakati wa kuwasilisha:**

Mwombaji anatakiwa kuonyesha yafuatayo:

- Hati ya Usajili ya Kampuni yake
- Leseni ya Biashara
- Namba ya Utambuzi wa Mlipa kodi (TIN)
- Kifaa cha fedha cha elektronik (EFD)
- Huduma alizokwisha kuzitoa katika Taasisi mbalimbali
- Idadi ya watumishi katika Kampuni yake na sifa walizo nazo.
- Orodha/Jedwali la huduma zilizotolewa na Kampuni katika vipindi vilivyopita
- Orodha ya vifaa ambavyo Kampuni inavitumia katika kutoa huduma.
- Uwezo wa kifedha wa Kampuni kwa ajili ya kuendesha huduma inayoombwa.
- Mpango kazi wa huduma anayoiomba.
- Maelekezo mafupi juu ya Kampuni (Company Profile) ambayo itakuwa halisi na nakala mbili.

Endapo kutakuwa na taarifa muhimu ambazo mwombaji anatakiwa kuzifahamu, ataziomba kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mara, S.L.P. 299, Musoma – sakafu ya kwanza chumba namba 24.

6. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni Ijumaa tarehe 16/06/2017 kabla ya saa 6.30 mchana. Kotesheni zitafunguliwa mbele ya wawakilishi wa Wazabuni watakaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa Zabuni katika *Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara*, Boma "A", Ukumbi mdogo S.L.P. 299, Musoma
7. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya Kotesheni, Kotesheni za ki-elektroniki na Kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji Kotesheni, kwa hali yoyote ile, Kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Adoh S. Mapunda
KATIBU TAWALA MKOA
MARA